# Shule ya E-Cubed

## KIJITABU CHA MAFANIKIO YA MWANAFUNZI

812 Branch Avenue
Providence, RI 02904
Simu ya mezani: 401-456-0694

Mkuu wa Shule: Dk. Matthew Juda
Mkuu wa Shule Msaidizi: Kerri Matheson

## Barua ya Kukaribisha


Karibu katika Shule ya E-Cubed, tumefurahi sana kuwa nawe kama mwanafunzi wetu mwaka huu wa masomo. Ni matumaini yangu kwamba utapata wakati mzuri na utakumbuka miaka hii kwa ufahari.

Kijitabu hiki ni mwongozo wako wa kufuata kwa matarajio, sera na taratibu za shule yetu. Hakikisha unapata muda wa kusoma taarifa hizo katika kurasa hizi kupata uelewa wa jinsi gani tunafanya kazi katika shule ya E-Cubed.

Wakati wako wa shuleni ni muda wa kukua na kujifunza. Nimefurahi umechagua E-Cubed kuwa mahali unaenda safari hii. Wewe sasa ni sehemu ya kitu maalum, kitu tofauti. Wewe ni sehemu ya familia ya Shule ya E-Cubed!

Hima Vijana Hodari!

Wako katika elimu,



Dk. Juda
Mkuu wa Shule
Shule ya E-Cubed

## Kitivo/Wafanyakazi wa E-Cubed ‘22-’23

**Mkuu wa Shule:** Dk. Matt Juda

Karani Kiongozi wa Shule: Helen Lanzourakis

**Mkuu wa Shule Msaidizi:** Bi. Kerri Matheson

Karani Mwandamizi wa Shule: Emanuella Petrucci

### Mwongozo:

Lin Taing (Mshauri Darasa la 9 na 12), Mwalimu Kiongozi

Melanie Nobles-Brunache (Mshauri Darasa la 10 na 11)

Karani Mwandamizi wa Mwongozo: Kimberly Robinson

### Mratibu wa Utamaduni wa Shule

Henock Constant

### Mtaalam Mwandamizi wa Jamii ya Shule

Tyler Dion

### Walimu wa Mafunzo

Roland Sasseville (Kusoma na Kuandika)

TBD- (Hisabati)

Melissa Rollings (Mwalimu wa Ushirikiano wa Mafunzo na Huduma Maalum)

### Sanaa:

Nicole Lepre, Mkuu wa Idara

Mia Dady

### Elimu ya Kazi na Ufundi

David Dekonski

Patricia Hill

Thomas Hoffman

## Masomo ya Sanaa ya Lugha ya Kiingereza

Donna Freeman
Alyssa Healey
Stephanie Morrison, Mwalimu Kiongozi
Michael Johnson

## Hisabati

Michael Eaton
Victoria Konovalenko
Sherrie Santos
Vivian Vargas

## Wanafunzi wa Lugha Mbalimbali

Joann Boss
Peter Breen, Mkuu wa Idara
Ronald DeSimone
Sengoudone Sengvilay

## Elimu/Afya ya Kimwili

Rebecca DelNigro
Daniel Damiano

## Sayansi

Mark Dibiasio
Alexander Major II, Mwalimu Kiongozi
Haley Ramos, Kiongozi wa Timu wa Darasa la 9
Fizikia - TBA

## Masomo ya Kijamii

Terrance Riordan
John Healy
Mark Manzo, Mwalimu Kiongozi
Joseph Styborski

Elimu Maalum

Kate Burakowski

Diana Ibarra-Sdoeung

Donald Izzo

Tempestt Philip

Marcia Ranglin-Vassell

Lugha za Dunia

Franz Delias

Louis DiSandro

Ellys Mattos, Mkuu wa Idara

Ivelisse Sabater

Mtaalam wa Vyombo vya Habari vya Maktaba:

TBD

Muuguzi wa Shule:

Elizabeth DaSilva

Mwalimu Msaidizi:

Nicole Bartels

Denise Kilpatrick

**Mfanyakazi wa Kijamii wa Shule:**

Katelynn Tewksbury

Mwanasaikolojia wa Shule:

TBD

Wafanyakazi wa Kifungoni:

Javier Lopez (Kiongozi)

Renita Harris

Ana Isabel Zuniga

Wafanyakazi wa Jikoni Sodexo:

Virgilia

Eugene

## Kauli ya Mpango wa Shule za Umma za Providence

Wilaya ya Shule ya Umma ya Providence itatayarisha wanafunzi wote kufaulu katika vyuo na vyuo vikuu vya kitaifa, na katika taaluma walizochagua**.**

## Kauli ya Maono ya Shule ya E-Cubed

Shule ya E-Cubed itakuwa jamii ya shule ya mfano ikiwaandaa wanafunzi WOTE kuwa hodari kwa lugha, werevu kitamaduni na walioendelea kitaaluma kwa matarajio makubwa, mafunzo mazuri na kuoneshwa mazingira ya mapema ya kazi na chuo yanayotolewa na wafanyakazi ambao wanakiri kuwa wanafunzi WOTE ni watu wa mabadiliko endelevu.

## Kauli ya Mpango wa Shule ya E-Cubed

Mpango wa Shule ya E-Cubed ni kuunda jamii yenye nguvu isiyo ya kibaguzi ambayo itaondoa vizuizi vyote katika kujifunza, hivyo kutumia uwezo wa kitaaluma, kijamii na kiraia wa wanafunzi wote.

## Maadili na Imani za Msingi

*Shule ya E-Cubed inaamini kwamba:*

- Kila mwanafunzi ni wa kipekee, hivyo kujifunza kunapaswa kuwe kwa bidii sana, kwa aina tofauti na kwa kuvutia.
- Wanafunzi, wazazi, wanajamii, na wanafunzi wana jukumu la pamoja kwa ajili ya kujifunza.
- Wanafunzi wapewe mwongozo na usaidizi wa shule na mipango ya kazi.

## Matarajio ya Shule za Umma za Providence

Kulingana na Shule za Umma za Providence' *Kanuni za Maadili ya Mwanafunzi:*

*Wanafunzi wana jukumu ku:*

- Fika shuleni kwa wakati, wakiwa wamejiandaa na tayari kujifunza;
- Kujiheshimu, kuheshimu wengine na mali;
- Kupanga kwa ajili ya baadaye mbeleni; na
- Kuomba msaada wakati unapohitajika.

## **Sera na Taratibu za Shule ya E-Cubed 2022-2023**

## Mahudhurio

Kulingana na *Kanuni za Maadili* ya Shule ya Umma ya Providence:
Mahudhurio ya shule ya kila siku ni kipengee muhimu katika mafanikio ya mwanafunzi ya kielimu na kijamii. Wanafunzi ambao wanahudhuria shuleni kila siku wanafanikiwa zaidi kielimu, kijamii na kihisia. Wana uwezekano mdogo kuacha shule na uwezekano mkubwa kuendelea na elimu yao zaidi ya sekondari.

Bodi ya Shule ya Providence inahitaji kwamba mwanafunzi yeyote ambaye ana utoro usio na sababu wa siku kumi (10) wakati wa muhula wa masomo au siku ishirini (20) wakati wa mwaka mzima wa masomo asipewe kozi au alama za darasani hadi aweze kuonyesha ustadi wa kozi ya darasa sawa na nyaraka ya mpango wa utendaji kitaaluma wa Shule ya Providence kama ilivyoamuriwa na mwalimu wa darasa.

- **Ulio na sababu:** utoro wowote uliothibitishwa kwa maandishi kutokana na ugonjwa, miadi ya matibabu, ushauri au mahakama; dharura ya familia au kifo; sikukuu za kidini, mikutano na matukio yaliyofadhiliwa na shule; na adhabu za kusimamishwa shule zilitolewa na shule.

- **Usio na sababu:** utoro wowote kutokana na likizo ya familia, ajira, mipango duni au kukatisha darasa. Kuchelewa mara tatu (3) bila sababu ni sawa na utoro mmoja (1) bila sababu.

## Taratibu kwa Utoro

Kwa tukio la utoro wa mwanafunzi:
- Mzazi/mlez anatakiwa kupiga simu katika ofisi kuu @ **401.456.0694** akiwa na sababu ya utoro.
- Ikiwa utoro zaidi unatarajiwa (siku tatu au zaidi) mzazi anapaswa kumwambia mshauri na aombe kuwasiliana na walimu wa mwanafunzi kwa ajili ya kazi za masomo za nyumbani.
- Wakati wa kurudi shuleni, mwanafunzi lazima alete taarifa kwa mshauri wa mwongozo au ofisini akionesha sababu ya utoro.

## Wachelewaji

Wanafunzi ambao ni wachelewaji shuleni *(muda wowote baada ya saa 2:55 ASUBUHI)* lazima wasaini na wapate karatasi nyeupe ya wachelewaji kutoka katika mashine ya kibanda cha wachelewaji mbele ya ofisi. Kikaratasi hiki lazima kiwasilishwe kwa mwalimu wakati wa kuingia darasani.

## Wachelewaji Darasani

Wanafunzi wanatarajiwa kuwa na kibali nyakati zote. Wanafunzi ambao ni wachelewaji watakuwa na kibali kutoka katika sehemu zao za awali wanapowasili darasani wakiwa wamechelewa.

- Kuchelewa darasani: wanafunzi wataonesha kibali cha sasa ili kuwasamehe kutokana na kuchelewa.
- Wanafunzi ambao wanawasili wakiwa wamechelewa darasani bila kibali watachukuliwa hatua za kinidhamu.
- Uchelewaji wa kurudia, hata ukiwa na kibali, unaweza kusababisha kupewa rufaa kwenda ofisini.

## Vibali vya Ukumbini

**Wanafunzi wote lazima wawe na kibali nyakati zote wakati hawajapangiwa kwenda darasani mwao.** Taratibu zifuatazo lazima zizingatiwe:

1. Vibali vinatolewa tu baada ya dakika 10 za mwanzo na kabla ya dakika 10 za mwisho za kipindi.
2. Kibali cha darasani kinatumiwa kwa ajili ya vyoo na kabati.
3. Kwa mwanafunzi kuenda ofisini, maktaba, kwenye mwongozo, mfanyakazi wa jamii, au muuguzi, mwalimu wao aliyepangwa lazima apige simu katika sehemu husika kupata ruhusa kabla ya kumtuma mwanafunzi. Wanafunzi hataruhusiwa kuingia bila ya kibali cha maandishi.
4. Wanafunzi wanatarajiwa kuwa katika madarasa yao waliyopangwa. Vibali visitolewe kuenda kwenye madarasa mengine.
5. Wanafunzi waliokutwa katika njia ya ukumbini bila kibali rasmi watarudishwa darasani na watahusika kwa hatua za kinidhamu

## Taratibu za Mavazi za Shule za Umma za Providence

*Kwa kuzingatia Kanuni za Maadili ya Mwanafunziza Wilaya ya Shule ya Umma ya Providence:*

- Chupi, mashati na blauzi lazima zisiwe zinaonesha/za kuona hadi ndani.
- Nguo za ndani za kuonesha au fulana/mashati mafupi (mashati ya kuonesha tumbo wazi) hayakubaliki.
- Kaptula na sketi lazima zishuke chini kwa urefu wa vidole vya mikono ikinyooshwa.
- Fulana na visidiria lazima vivaliwe na shati lenye mikono.
- Nguo za kubana zinaruhusiwa katika madarasa ya elimu ya viungo vya mwili tu.
- Vitambaa vya kufunika uso, vifaa na nguo za magenge ambavyo vinaonesha lugha za matusi na tabia chafu, vinavyochochea vurugu au matumizi ya madawa ya kulevya, vileo au tumbaku, au vina viashiria vya ngono haviruhusiwi.
- Maneno au picha kwenye nguo zisiwe zile zisizo faa au kutangaza pombe, madawa ya kulevya au ushirika na magenge
- Wanafunzi wanaoshiriki katika elimu ya viungo vya mwili waruhusiwe kuvaa rangi yoyote ya kaptula au suruali za michezo na tisheti bila adhabu.

Wanafunzi wanatarajiwa kuwasiliana na mzazi/mlezi kuleta mabadiliko ya nguo ambayo yanaendana na taratibu za mavazi za wilaya. Wanafunzi watapewa adhabu ya kubaki shuleni kwa muda kufidia muda wa mafunzo uliopotea.

## Kabati

- Kila mwanafunzi katika shule ya E-Cubed atapewa kabati kwa muda wote wa miaka minne.
- Wanafunzi wanatakiwa kutumia makufuli yaliyotolewa na shule. Kufuli lolote ambalo halijatolewa na E-Cubed litakatwa na kuondolewa kutoka katika kabati.
- Makufuli yote lazima yafungwe wakati hayatumiki.
- Wanafunzi wasichangie kabati na wanafunzi wengine.
- Chakula lazima kitolewe kutoka katika kabati kila siku.
- Kuchafua kwa aina yoyote kwa kuandika kwenye kabati kutaleteleza/kutasababisha kupewa adhabu ya kubaki shuleni. Mwanafunzi atawajibika kusafisha kabati kwa wakati huo.
- Hakutakuwa na kupewa tena kabati.
- Kabati za mazoezi ya viungo vya mwili hazijagawiwa na zipo kwa matumizi wakati wa mazoezi ya viungo vya mwili tu. Wanafunzi wanaruhusiwa kuleta makufuli yao wenyewe lakini lazima wayaondoe mwisho wa masomo. **Makufuli yote yaliyoachwa kwenye kabati za mazoezi ya mwili yataondolewa.**
- Upewaji kabatina uchanganyaji unapatikana katika Skyward
- Wanafunzi wanatarajiwa kufungua kabati zao mwanzo wa siku, na mwisho wa siku na vipindi kati ya masomo, ikiwa muda unaruhusu.
- Ikiwa mwanafunzi anahitaji kutumia kabati lake wakati wa kipindi cha masomo, lazima waombe walimu wao ruhusa na watumie kibali cha darasani.

## Sera ya Vifaa vya Kielektroniki

Matumizi mabaya ya teknolojia yanazuia mazingira ya kujifunza na yanaathiri ubora wa kujifunza darasani.

1. Simu zinatarajiwa kuwekwa kwa usalama (katika begi la mgongoni, kabatini, mfukoni n.k.) na zisitumiwe wakati wa muda wa masomo **hadi pale** zitakaporuhusiwa na mwalimu kwa matumizi katika masomo ya darasani.
2. Wanafunzi hawaruhusiwi kuondoka darasani ili kupokea miito ya simu. Wazazi/Walezi wanaweza kupiga simu ofisini ikiwa wanahitaji kuwasiliana na mtoto wao.
3. **Kwa madhumuni ya usalama na ulinzi:**
    a. Miito ya video hairuhusiwi kwenye viwanja vya shule
    b. Kurekodi video au kupiga picha wanafunzi wengine bila ruhusa yao kunakatazwa vikali
4. Simu za mkononi haziruhusiwi wakati wa mitihani ya majaribio, hasa lakini si tu kwa PSAT, SAT, NGSA, ACCESS na mitihani ya majaribio ya AP. Mwanafunzi yeyote atayepatikana na simu wakati wa mitihani ya majaribio ana hatari ya kufutiwa matokeo yake na kufukuzwa asirudie mitihani.
5. Kushindwa kuendana na ombi la mwalimu/mfanyakazi yeyote katika suala hili kutachukuliwa sawa na kukataa kutii amri na kutashughulikiwa kulingana na Kanuni za Maadili ya Mwanafunzi.

## Sera ya Chakula na Vinywaji

Uagizaji na uletaji wa chakula unakatiza jamii ya kujifunza. Kutokana na usalama wa shule, vitu vyenye kuleta mzio, na mikataba iliyopo pamoja na watoa huduma, **uletaji wa chakula <u>hauruhusiwi</u>.** Wanafunzi wana haki ya kupata kifungua kinywa na chakula cha mchana wakati wa siku ya masomo.

## Kuondoka Mapema

- Watu wote walioidhinishwa walioorodheshwa kwenye Fomu ya Dharura lazima wawe na miaka 18 au zaidi.

- Wakati mzazi/mwanafamilia aliyeorodheshwa kwenye Fomu ya Dharura anapokuja kumchukua mwanafunzi kwa ajili ya kuondoka mapema, wanatakiwa kuripoti moja kwa moja kwenye ofisi kuu. Wazazi/Walezi wasiruhusiwe kuenda kwenye madarasa ya wanafunzi au maeneo mengine yoyote ya jengo.

- Wafanyakazi wa ofisi wataomba fomu kamili ya KITAMBULISHO chenye picha. Ikiwa mtu aliyeorodheshwa hana KITAMBULISHO, wataombwa kwenda kuchukua **kabla** mwanafunzi hajaruhusiwa kwao.

- KITAMBULISHO chenye picha lazima kifanane na mtu anayekitoa na jina kwenye KITAMBULISHO lazima lifanane na jina lililoorodheshwa kwenye fomu ya Dharura. Vinginevyo, mwanafunzi **hata**achiliwa kwao.

- Kabla ya kuondoka, mwanafunzi lazima asainiwe kuwa ametoka katika kitabu cha kuandikisha.
- Kuondoka mapema kukizidi kunaweza kusababisha hatua ya kinidhamu

# <u>Taratibu za Dharura</u>

## Mazoezi ya Kuzima Moto

- Wakati wa mazoezi ya kuzima moto, wanafunzi lazima wawe na mwalimu wao wa darasa waende kimya kupitia kumbini, waache jengo kupitia darasa lao walilopewa kwenye **mlango wa kutokea.**
- Wanafunzi watafuata taratibu za kutoka za mfano zinazofaa na salama kutoka kwa walimu.
- Wanafunzi/wafanyakazi wanaondoka kutoka mlango 1, 3 na 8 wataelekea kwenye sehemu ya maegesho ya kanisa, huku wanafunzi/wafanyakazi wakiondoka kutokea mlango 6 watapanga mstari kwenye sehemu ya kutembea kwa miguu kwenye Mtaa wa Burleigh
- Wanafunzi wanatarajiwa kukaa na walimu wao nyakati zote na mahudhurio yataangaliwa na walimu kwa kutumia matangazo mekundu/manjano/kijani.

Wanafunzi watazingatia sera ya kutoongea ili kuruhusu mafundisho yasikike vizuri na wote waliopo.

**Mazoezi ya Kuzima Moto yasiishe hadi wanafunzi wote wawe katika madarasa yao waliyopewa.**

Kulingana na njia za mazoezi ya kuzima moto zilizotolewa, zifuatazo zinatolewa:

1. Wanafunzi/wafanyakazi katika vyumba 118A, 118B, 120, 129, 131, Ofisi ya Walimu, na Ofisi nyingine watatoka katika jengo kupitia Mlango wa kutokea 1
2. Wanafunzi/wafanyakazi katika vyumba - Mazoezini, vyumba vyenye Kabati, 121, 122, 140, 141 na Jikoni watatoka kupitia Mlango 3.
3. Wanafunzi/wafanyakazi katika vyumba 173, 172, 150, 139, 141, 149, na Mgahawani watatoka kupitia Mlango 6.
4. Wanafunzi/wafanyakazi katika vyumba 145, 146, 147, 148, Maktaba, na137 watatoka kupitia Mlango 8.
5. Wanafunzi ambao hawako darasani mwao lazima watafute mlango wa kutokea ulio karibu na waungane na wenzao. Walimu wataonesha jambo hili kwa kutumia tangazo la rangi sahihi kama ilivyoelezwa hapo juu.

## Utaratibu wa Kaa Chonjo

Ikiwa "KAA CHONJO" inasikika kwenye mfumo wa matangazo:

- Walimu na wanafunzi watabaki katika madarasa yao waliyopewa au watarudi kwenye vyumba vyao walivyopewa.
- Wanafunzi watabaki katika madarasa bila vurugu na watasubiri maelekezo zaidi kwenye mfumo wa matangazo.

## Hali ya Kuweka Salama Jengo

Hali ya Kuweka Salama Jengo itatangazwa kwenye mfumo wa matangazo ikiwa kuna tatizo la kiusalama linahisiwa nje ya jengo ambalo linaweza kuingilia masomo ya wanafunzi.

- Wanafunzi wata**baki katika madarasa yao waliyopangiwa na milango yao ikiwa imefungwa**
- Hakuna vibali vitatolewa kwa wanafunzi
- Maelekezo ya darasani yataendelea
- Hali ya Kuweka Salama Jengo itabaki ikitekelezwa hadi msimamizi au afisa wa polisi atakapotoa taarifa kwamba shughuli za kawaida zinaweza kuendelea.

## Utaratibu wa Ngambi Kutotoka Nje

Jengo la shule litakuwa chini ya amri ya kutotoka nje wakati hali inayohisiwa inapotokea ambayo inaweza kuathiri usalama wa shule yetu.

Wasimamizi wa Shule ya E-Cubed watatangaza mwanzo wa ngambi kutotoka nje kwenye mfumo wa matangazo ya hadhara. Wanafunzi na wafanyakazi watasikia tangazo.

1. Wanafunzi wanataripoti/watakaa na mwalimu wao waliyepangiwa.
2. Ikiwa mwanafunzi hayuko na mwalimu, wanatakiwa kutafuta mwalimu aliye karibu au msimamizi ili wachukuliwe kupelekwa mahali salama
3. Madirisha ya kufumba/ya kuziba lazima yafungwe.
4. Kila mmoja lazima awe kimya na simu ziwe katika hali ya ukimya.

5. Hakuna mtu kujibu **mawasiliano yoyote kutoka nje** hadi msimamizi au afisa wa polisi aruhusu darasa yeye mwenyewe.
6. Usiondoke mahali pako salama hadi uelekezwe na msimamizi au afisa wa polisi yeye mwenyewe.

## Taratibu za Uokoaji Watu

*Utaratibu wa mazoezi ya kuzima moto utatumika pia kwa ajili ya mazoezi ya Uokoaji watu.*

- Wanafunzi lazima wawe na mwalimu wao wa darasa waende kimya kupitia kumbini, waache jengo kupitia **mlango wa kutokea** wa darasa lao walilopewa.
- Wanafunzi watafuata taratibu salama za kutoka zinazofaa kutoka kwa walimu na watawasili kuripoti katika Kiwanja cha Maegesho cha Mtaa wa Veazie na watajipanga mstari *na wenzao wa darasa* katika maegesho.
- Wanafunzi ambao hawako darasani mwao lazima watafute mlango wa kutokea ulio karibu na waungane na wenzao.
- **Sehemu za kutembea kwa miguu lazima zitumike nyakati zote**
- **Tafadhali kaa kimya ili kusikia maelekezo**


Milango ya Kutokea na Mpango wa Uokoaji:

- Wakati wa kutoka katika jengo, wanafunzi na wafanyakazi watatembea katika Mtaa wa Veazie, watakata kushoto katika Mtaa wa Shiloh, na wataendelea mojamoja katika kiwanja cha Maegesho cha Veazie.
  - Wanafunzi/wafanyakazi katika vyumba 118A, 118B, 120, 129, 131, Ofisi ya Walimu, na Ofisi nyingine watatoka katika jengo kupitia Mlango wa kutokea 1
  - Wanafunzi/wafanyakazi katika vyumba - Mazoezini, vyumba vyenye Kabati, 121, 122, 140, 141 na Jikoni watatoka kupitia Mlango 3.
  - Wanafunzi/wafanyakazi katika vyumba 145, 146, 147, 148, Maktaba, na137 watatoka kupitia Mlango 8.

- Wanafunzi/wafanyakazi katika vyumba 173, 172, 150, 139, 141, 149, na Mgahawani watatoka kupitia Mlango 6; kisha wataenda kulia kwenye Mtaa wa Burleigh, kisha watageuka kushoto kwenye Mtaa wa Winchester, kisha watakata kulia kwenye Mtaa wa Hyacinth, ambao utawapeleka kwenye Maegesho ya Veazie upande wa mkono wa kushoto.

*Wafanyakazi na wanafunzi wote watafuata njia ya Mtaa wa Shiloh kurudi kwenye jengo na wote wataingia tena ndani kupitia milango mikuu*

## Ramani ya Jengo 2022-23




## Hali Mbaya ya Hewa, Ufungaji Shule wa Dharura, Kuondoka Mapema na Kuchelewa

*Hakutakuwa na tangazo ikiwa saa za shule hazibadilishwi katika kalenda ya shule.*

Ikitokea saa za kazi zilizopangwa za shule zitabadilika, taarifa kuhusu mabadiliko zinaweza kupatikana katika njia zifuatazo:

- Wazazi wataarifiwa kupitia "Kinvo au Kiungo cha Wazazi" cha wilaya cha mfumo wa ujumbe wa simu. **Tafadhali hakikisha wanafunzi na wazazi wana Taarifa sahihi za Mawasiliano ya Dharura kwenye faili la shule.**
- Taarifa zitachapishwa kwenye tovuti ya shule
- Kufunga shule, kuahirisha, na kuchelewa kunapatikana kwenye njia zifuatazo za vyombo vya habari zikishirikiana na Chama cha Watangazaji cha Kisiwa cha Rhode pia zimethibitishwa na Vyombo vya Mitandao ya Kijamii:

**Televisheni:**
WLNE (ABC – Chaneli 6)

WJAR (NBC – Chaneli 10)
WPRI (CBS – Chaneli 12)
WSBE (PBS – Chaneli 36)
Telemundo 50 (Kihispania)
WNAC (FOX – Chaneli 64)

**Redio ya FM:**
WELH FM 88.1
WPRO FM 92.3
WSNE FM 93.3
WHJY FM 94.1
WBRU FM 95.5
WCRI FM 95.9
WCTK FM 98.1

WJZS FM 99.3
Latina FM 100.3 (Kihispania)
WWBB FM 101.5
WRNI FM 102.7
WEEI FM 103.7
WWLI FM 105.1
WWKX FM 106.3

**Redio ya AM:**
WPRO AM 630
WSKO AM 790
WHJJ AM 920
WPMZ AM 1110 (Kihispania)
WOON AM 1240
WRNI AM 1290 (Kihispania)
WNBH AM 1340
WNRI AM 1380
WADK AM 1540
WARV AM 1590

*Familia na wanafunzi wanaweza kujisajili kupata taarifa za HUDUMA YA UJUMBE MFUPI kutoka katika Watangazaji wa Kisiwa cha Rhode kwa kutembelea [https://www.ribroadcasters.com/](https://www.ribroadcasters.com/) na kuchagua "Jisajili kwa Taarifa." Tafadhali chagua **Shule za Sekondari za Umma za Providence** ili kupokea taarifa za shule ya E-Cubed.*

## Taratibu za Maktaba za Shule za Umma za Providence

**Matumizi ya Maktaba** – Maktaba ipo wazi kwa wanafunzi kwa ajili ya kufanyia kazi za masomo, miradi na kupata vitu vya kujisomea. Wanafunzi wanaweza kuja Maktaba wanapokuwa na ruhusa kutoka kwa mwalimu waliyepangiwa. Walimu watamuita/watampigia simu Mkutubi na kuandika kibali kwa ajili ya mwanafunzi. Wanafunzi wanaweza kupata kibali kutoka kwa mwalimu au mshauri wakati wanapopangwa kwa mwalimu au mshauri huyo. Wanafunzi wanaweza kutumia maktaba ikiwa hakuna masomo yanayofanyika katika sehemu hiyo na kwa usimamizi wa wafanyakazi.

**Vitabu Vinavyozunguka -** Wanafunzi wanaweza kuazima vitabu kwa majuma matatu na hiari ya kuongeza muda wa kuazima kwao kwa majuma matatu mengine. Ili kuongeza muda wa kuazima kitabu, mwanafunzi lazima alete kitabu Maktaba ili kuongeza muda tena. Wanafunzi hawataweza kuazima vitabu ikiwa hawajarudisha kitabu ambacho muda wake umepita au wamerudisha kitabu kimeharibiwa. Wanafunzi hawataweza kuazima vitabu ikiwa wanadaiwa vitabu kwenye maktaba nyingine yoyote ya shule ya umma ya Providence.

**Sera kwa Kitabu Kilichopotea -** Wanafunzi hawataweza kuazima vitabu ikiwa wamepoteza vitabu vya maktaba ya shule au hawajarudisha vitabu vya maktaba. Wanafunzi wanawajibika kulipa kwa vitabu vyovyote vya maktaba vilivyopotea au kuharibiwa. Malipo yanafanyika kwa Mkutubi wa Shule. Wanafunzi wanaohitimu hawatapata stashahada zao hadi vitabu vyao vilivyopotea vilipwe. Wanafunzi wanaohitimu au wanaohama hawatapata rekodi za

shule au rekodi za shule kutumwa kwenda shule zingine hadi vitabu vilivyopotea vilipwe. Wanafunzi wanaweza kufukuzwa kutoka katika shughuli za mwisho wa mwaka ikiwa hawajalipa vitabu vya maktaba vilivyopotea. Wanafunzi hawataweza kuazima vitabu ikiwa wanadaiwa vitabu vingine vyovyote. Mkutubi wa Shule atatuma malipo kwa vitabu vilivyopotea kwa maktaba ya shule husika.

## Sera ya Chromebook na Teknolojia

**Chromebooks**

- Kila mwanafunzi atapatiwa na atapewa chromebook na chaja mwanzoni mwa kujiandikisha kwao katika Shule ya E-Cubed.
- Wanafunzi wataingia kwenye chromebook zao kwa anuani za baruapepe za shule zao na kutengeneza nenosiri
- Ikiwa mwanafunzi anasahau neno siri lao, wanaweza kulipata kutoka katika Mratibu wa Utamaduni ofisini
- Wanafunzi hutunza chromebook na chaja zao kwa kipindi chote cha kuwapo kwao katika Shule ya E-Cubed.
    - Ikiwa mwanafunzi anahamia shule nyingine, wanatakiwa kurudisha chromebook na chaja zao kwa Mratibu wa Utamaduni ofisini
- Wanafunzi wanatarajiwa kurudisha chromebook na chaja zao kwa Mratibu wa Utamaduni mwishoni mwa kila mwaka wa masomo wa shule
    - Ikiwa wanafunzi wanahitaji Chromebook kwa masomo msimu wa kiangazi au mpango wa kufanana na huo lazima wapate ruhusa kutoka kwa Mratibu wa Utamaduni ili kuchukua.

**Ukarabati wa Chromebook:**

Chromebook ambazo zinahitaji ukarabati lazima ziletwe kwa Mratibu wa Utamaduni ili ziweze kupelekwa nje kwa ukarabati

- Wanafunzi watapata chromebook nyingine ya kuazima kwa kipindi cha ukarabati
- Wanafunzi lazima warudishe hii ya kuazima wakati wa kumaliza ukarabati

- *Chromebooks za kuazima zinatolewa kwa wanafunzi wale tu ambao wana Chromebook zinakarabatiwa.*

**<u>Chaja za Chromebook</u>**

Chaja za kufidishia zipo kiasi kidogo sana.

- Ikiwa mwanafunzi anapoteza chaja zao, wanawajibika kufidishia.
- Ikiwa chaja imeharibika, mwanafunzi apeleke chaja kwa Mratibu wa Utamaduni, ambaye ataamua ikiwa mwanafunzi anahusika kufidishia
- Ikiwa mwanafunzi anasahau chaja zao kwa siku hiyo, au hana chaja, wanaweza kutumia sehemu ya kuchajia katika mgahawa **wakati wa chakula cha mchana**

*Ikiwa mwanafunzi anasahau chromebook yao siku hiyo, wanatarajiwa kutumia kompyuta ya mezani katika kila chumba cha darasa. Wanafunzi wataingia kwenye kompyuta hizi kwa anuani za barua pepe na nenosiri za shule zao.*

**<u>Sera kwa Chromebook Iliyopotea -</u>**

Kwa Chromebook ambayo imepotea au imeibiwa, Ripoti kwa Polisi lazima ipatikane na mzazi au mlezi. Nakala ya Ripoti ya Polisi lazima itolewe kwa Mratibu wa Utamaduni.

- Wanafunzi ambao wanapoteza chromebook na hawastahili kupewa nyingine watapatiwa chromebook ya kuazima mumo humo ndani.
- Wazazi/walezi na Wanafunzi wanawajibika kufungua ripoti polisi.

## MAHITAJI YA KUHITIMU

Mahitaji ya kuhitimu ya wilaya yanataka kwamba wanafunzi wafaulu si chini ya kozi <u>21</u> katika nyanja za masomo husika ya msingi, ambayo yanaweza kubadilika kulingana na Idara ya Elimu ya Wilaya ya Shule ya Providence na Kisiwa cha Rhode. Hali kadhalika, wanafunzi wa Shule ya E-Cubed lazima wakamilishe alama zinazotakiwa za kozi ya CTE ili wafuzu ajili ya kuhitimu.

| # Alama Zinazotakiwa | Kozi | Mahitaji ya Ziada |
|---|---|---|
| 4 | Kiingereza | Mitihani ya Mwisho wa Kozi<br><br>Tathmini ya Stashahada Kutegemea Utendaji (PBDA)<br><br>PSAT10 & SAT<br><br>NGSA (tathmini ya Sayansi) |
| 4 | Hisabati | |
| 3 | Historia | |
| 3 | Sayansi | |
| 2 | Elimu/Afya ya Kimwili | |
| 2 | Lugha ya Dunia *(lugha ile ile)* | |
| | Kompyuta (CTE) * | |
| 0.5 | Sanaa | |
| 0.5 | Kozi za masomo ya hiari | |
| 2 | | |

* Darasa la 2025 lazima likamilishe mfululizo wa kozi 4 za CTE

- **Darasa la Tisa:** Ili kupandishwa darasa kutoka la 9 kwenda la 10 wanafunzi lazima wafaulu si chini ya kozi zao tatu za msingi **na** lazima wawe wamekamilisha vizuri alama 5 kwa kiwango cha chini
- **Darasa la Kumi:** Ili kupandishwa darasa kutoka la 10 kwenda la 11 wanafunzi lazima wafaulu si chini ya kozi zao sita za msingi **na** lazima wawe wamekamilisha vizuri alama 10 kwa kiwango cha chini.
- **Darasa la Kumi na Moja:** Ili kupandishwa darasa kutoka la 11 kwenda la 12 wanafunzi lazima wawe wamekamilisha alama 16 zikiwamo alama 3 kwenye somo la Kiingereza na 3 kwenye Hisabati.
- **Darasa la Kumi na Mbili:** Ili kuhitimu mwanafunzi lazima awe na **kiwango cha chini** cha 21 **zinazotakiwa** alama za kuhitimu, **PAMOJA NA** kukamilisha mahitaji yote mengine ya Shule ya E-Cubed na ya wilaya ikiwamo PBDA, SAT, Mitihani ya Mwisho wa Kozi

***** Mahitaji ya Kuhitimu kwa Darasa la 2026 yanangojea Idara ya Elimu ya Kisiwa cha Rhode uthibitisho *****

## Daraja la Darasa

- Uwekaji madaraja kwenye jedwali unakokotoa G.P.A ya mwanafunzi unawekwa kwenye mfumo wa kompyuta ya shule. Katika kukokotoa G.P.A ya mwanafunzi jedwali linajumuisha vipengee kadhaa, kama vile alama zilizopatikana kwa kila kozi (0-100), thamani ya alama za kozi (kozi za Heshima na kozi za Uwekwaji Daraja la Juu zina thamani kubwa) na thamani husika iliyokokotolewa kwa kozi zilizopewa alama ya kufaulu/kufeli.
- G.P.A na Madaraja ya Darasa yanatumika kwa wanafunzi ambao wameandikishwa katika Shule ya E-Cubed kwa angalau mwaka mmoja mzima wa masomo.
- **Kufuzu kwa hadhi ya Kumi Bora wanafunzi lazima wawe wameandikishwa katika shule ya E-Cubed kwa angalau mihula sita.**
- Madaraja ya G.P.A ya mwisho na ya Darasa yanaamuriwa mwishoni mwa robo ya 3 ya mwaka wa mwisho wa kuhitimu.

| Mfumo wa alama ufuatao utaamuriwa mwishoni mwa mwaka wa mwisho wa kuhitimu: | |
|---|---|
| 1. GPA ya kuongezeka | • inaamuriwa mwishoni mwa robo ya 3 ya mwaka wa mwisho wa kuhitimu.<br>• Wahitimu wa kumi bora watapangwa madaraja kwa GPA na watapewa idadi ya alama zifuatazo.<br>○ wa 1: Alama 30; wa 2: Alama 27; wa 3: Alama 24; wa 4: Alama 21; wa 5: Alama 18; wa 6: Alama 15; wa 7: Alama 12; wa 8: Alama 9; wa 9: Alama 6; wa 10: Alama 3<br>○ Hii inakuwa na jumla ya asilimia 60%. |
| 2. Masomo ya Juu | • Idadi ya masomo ya juu yaliyochukuliwa wahitimu wa daraja la kumi bora yataamuriwa mwishoni mwa robo ya tatu ya mwaka wa mwisho wa kuhitimu.<br>• Hizi ni pamoja na: Fasihi AP, Historia ya Marekani, Siasa na Serikali AP, Lugha ya Kihispania AP, Hisabati za Calculus za Awali, Biolojia AP, Kujiandikisha Masomo Pawili, AP Sanaa ya 2D AP, Kujiandikisha Masomo Pawili, Kihispania III, na Mtandao wa Kozi ya Juu. |

| | |
|---|---|
| | ○ Idadi ya alama zifuatazo zinaamuriwa: wa 1: Alama 10; wa 2: Alama 9; wa 3: Alama 8; wa 4: Alama 7; wa 5: Alama 6; wa 6: Alama 5; wa 7: Alama 4; wa 8: Alama 3; wa 9: Alama 2; wa 10: Alama 1<br>○ Hii inakuwa na jumla ya asilimia 20%. |
| 3. Matokeo ya SAT | ● Matokeo ya mwisho ya SAT yaliyofikiwa na wahitimu wa kumi bora yataamuriwa mwishoni robo ya tatu ya mwaka wa mwisho wa kuhitimu.<br>● Shule itapitia upya matokeo ya mwisho yaliyotolewa kabla ya mwisho wa Januari.<br>○ Alama zifuatazo zitazingatiwa kwa wahitimu wa kumi bora. wa 1: Alama 10; wa 2: Alama 9; wa 3: Alama 8; wa 4: Alama 7; wa 5: Alama 6; wa 6: Alama 5; wa 7: Alama 4; wa 8: Alama 3; wa 9: Alama 2; wa 10: Alama 1<br>○ Hii inakuwa na jumla ya asilimia 20% |

Jumla kutoka katika #1 - #3 zitatumika kuchagua mwanafunzi wa kwanza na mwanafunzi wa pili. Mkuu wa washauri wa shule wanatoa uamuzi wa mwisho ni watu ambao watazungumza wakati wa kuhitimu na/au wakati wa sherehe ya kutoa zawadi kwa wahitimu. Hotuba za wanafunzi kwa sherehe hizi lazima zihakikiwe kwanza. Mkuu wa Shule na Mshauri wa Mwongozo watakutana na wanafunzi kumi bora na kuwaarifu kuhusu heshima hii na kuanza kujiandaa kwa ajili ya kuhitimu.

## Sera ya Uzima Kimwili

**Kuimarisha na kuendeleza uzima kimwili:**
Wanafunzi ambao wameandikishwa katika Shule ya E-Cubed lazima wazingatie matakwa ya shule, wilaya na ya ligi ya wanafunzi ya Kisiwa cha Rhode ili wawe na sifa ya kushiriki michezo ya kimwili na riadha.

- **Matarajio ya Jamii:** Dumisha matarajio kuhusu mwenendo mzuri wa wanafunzi shuleni, na kwenda na kutoka shuleni; ikiwa ni pamoja na kutumia Mitandao ya Kijamii ipasavyo
- **Matarajio ya Mahudhurio:** Dumisha mahudhurio yanayokubalika
  - Wanafunzi lazima waje shuleni kwa wakati *na* kwa siku nzima ili kuhudhuria mazoezi au michezo
  - Utoro kupita kiasi na/au kuchelewa kunaweza kusababisha mwanafunzi kutostahiki muhula huo
- **Matarajio ya Kitaaluma:** Wanafunzi wanatarajiwa kuwa katika msimamo mzuri wa kitaaluma. Ustahiki wa kitaaluma kwa michezo ya Majira ya Baridi na Majira ya Kuchipua huamuriwa na *kadi ya ripoti ya robo ya awali.* Mahitaji ya kitaaluma ya michezo ya Msimu wa Kupukutisha Majani yanategemea *alama za mwisho kutoka mwaka uliopita.* Kozi zozote za shule msimu wa kiangazi au za kupata upya alama za mitihani lazima zikamilishwe kabla ya msimu wowote kuanza. Wanafunzi lazima wafanye asilimia 67% ya kozi za alama za mitihani ili waendelee kustahiki kuwa na sifa.

*Utawala katika Shule ya Sekondari ya Hope au E-Cubed kila moja ina haki ya kuwanyima wanafunzi kushiriki katika riadha hata kama wanastahiki.*

**Matakwa na Wajibu:**
- Wanafunzi wanahimizwa kuwasilisha ratiba, kamili na maelezo ya kocha wao, kwa Mkuu wa Shule Msaidizi
- Mawasiliano ya uwazi kuhusu mabadiliko ya ratiba yanapaswa kutokea mara kwa mara.

## Timu za Michezo ya Kishule (Ushirikiano na Shule ya Sekondari ya Hope)

| **Michezo ya Msimu wa Kupukutisha Majani** | **Michezo ya Msimu wa Majira ya Kipupwe** | **Michezo ya Msimu wa Kuchipua Majani** |
|---|---|---|
| Mashindano ya Mbio Ndefu ya Wavulana | Mpira wa Kikapu wa Wavulana | Mpira wa Bezi wa Wavulana |
| Mashindano ya Mbio Ndefu Wasichana | Mpira wa Kikapu wa Wasichana | Mpira Laini wa Wasichana |
| Soka Wavulana | Riadha za Uwanja wa Ndani za Wavulana | Riadha za Uwanja wa Nje za Wavulana |
| Soka Wasichana | Riadha za Uwanja wa Ndani za Wasichana | Riadha za Uwanja wa Nje za Wasichana |
| Tenisi Wasichana | Mieleka | Mpira wa Kikapu wa Pamoja Wazima na Wenye Ulemavu |
| Mpira wa Voli wa Wasichana | Mpira wa Kikapu wa Wavulana wa Mwaka wa Kwanza | Michezo ya E (Mpya!) |
| Mpira wa miguu | | |
| Michezo ya E (Mpya!) | | |

## Sherehe/hafla za Kijamii za Mwaka wa Mwisho wa Kuhitimu na Shule nzima

Kuhudhuria sherehe/hafla za kucheza muziki za mwaka wa mwisho wa kuhitimu na sherehe zingine ni fursa nzuri. Fursa ya kushiriki katika hafla hizi hutolewa kwa wanafunzi ambao wanakidhi matarajio.

**Matarajio ya Jumla:**

Ni muhimu kwa wanafunzi kudumisha tabia nzuri na inayofaa ambayo haizuii kitu katika mazingira ya kusoma katika shule ya E-Cubed.

- **Matarajio ya Jamii:** Dumisha matarajio kuhusu mwenendo mzuri wa wanafunzi shuleni, na kwenda na kutoka shuleni; ikiwa ni pamoja na kutumia Mitandao ya Kijamii ipasavyo. Tabia nzuri na inayofaa inaweza kufika hadi kwenye *mzozo wowote ambao unatokea nje ya shule na unaendelea kuathiri jamii ya shule yetu.* Haya yanaweza kujumuisha mawasiliano katika mitandao ya kijamii au nje ya maeneo ya shule. Wanafunzi wanahimizwa kuenenda wenyewe kwa namna ya kitaalam.

- **Matarajio ya Mahudhurio:** Dumisha mahudhurio yanayokubalika
    - Wanafunzi lazima waje shuleni kwa wakati *na* kwa siku nzima ili kuhudhuria hafla za kijamii isipokuwa kama wameagizwa vinginevyo na utawala
    - Utoro kupita kiasi na/au kuchelewa kunaweza kusababisha mwanafunzi asistahiki hafla

- **Matarajio ya Kitaaluma:** Wanafunzi wanatarajiwa kuwa katika msimamo mzuri wa kitaaluma. Wanafunzi wanaohudhuria hafla hizi lazima wawe wamelenga kupandishwa daraja kwenda ngazi nyingine ya daraja na wawe wameshiriki katika matakwa yoyote ya ziada kwa daraja lao la sasa (mfano: PBDA, SAT, NGSA). Hali kadhalika, Wanafunzi lazima wawe wamefaulu (angalau ustadi wa 60%) katika kila darasa ili waweze kustahiki kushiriki

*Usimamizi katika Shule ya E-Cubed una haki ya kuwazuia wanafunzi kushiriki katika hafla za shule kwa kushindwa kuzingatia matarajio hapo juu.*

## Ratiba ya Mwanzo wa Vipindi kwa 2022-23

# E-Cubed Academy

| Bell Schedule 2022-23 | | | |
|---|---|---|---|
| Period | Start Time | End Time | Duration |
| 1 | 8:50 AM | 9:50 AM | 60 Min |
| 2 | 9:53 AM | 10:53 AM | 60 Min |
| 3 | 10:56 AM | 11:56 AM | 60 Min |
| 4 | 11:59 AM | 1:29 PM | 90 Min |
| **LUNCH A**-Rooms: 145, 146, 147, 148, 149, 150, 132 | | | |
| Lunch | 11:59 AM | 12:26 PM | 27 Min |
| Class | 12:29 PM | 1:29 PM | 60 Min |
| **LUNCH B**-Rooms: 137, 139, 140, 141, 171, 172, 173 | | | |
| Class | 11:59 AM | 12:29 PM | 30 Min |
| Lunch | 12:30 PM | 12:57 PM | 27 Min |
| Class | 12:59 PM | 1:29 PM | 30 Min |
| **LUNCH C**-Rooms: 118B, 120, 121, 122, 129, 131, Gym | | | |
| Class | 11:59 AM | 12:59 PM | 60 Min |
| Lunch | 1:02 PM | 1:29 PM | 27 Min |
| 5 | 1:32 PM | 2:32 PM | 60 Min |
| 6 | 2:35 PM | 3:35 PM | 60 Min |

| Advisory Schedule | | | |
|---|---|---|---|
| Period | Start Time | End Time | Duration |
| 1 | 8:50 AM | 9:38 AM | 48 Min |
| 2 | 9:41 AM | 10:29 AM | 48 Min |
| 3 | 10:32 AM | 11:20 AM | 48 Min |
| 4 | 11:23 AM | 12:53 PM | 90 Min |
| **LUNCH A**-Rooms: 145, 146, 147, 148, 149, 150, 132 | | | |
| Lunch | 11:23 AM | 11:50 AM | 27 Min |
| Class | 11:53 AM | 12:53 PM | 60 Min |
| **LUNCH B**-Rooms: 137, 139, 140, 141, 171, 172, 173 | | | |
| Class | 11:23 AM | 11:53 AM | 30 Min |
| Lunch | 11:54 AM | 12:21 PM | 27 Min |
| Class | 12:23 PM | 12:53 PM | 30 Min |
| **LUNCH C**-Rooms: 118B, 120, 121, 122, 129, 131, Gym | | | |
| Class | 11:23 AM | 12:23 PM | 60 Min |
| Lunch | 12:26 PM | 12:53 PM | 27 Min |
| 5 | 12:56 PM | 1:44 PM | 48 Min |
| Advisory | 1:47 PM | 2:44 PM | 57 Min |
| 6 | 2:47 PM | 3:35 PM | 48 Min |

| | Daily Rotations | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | P | A | N | T | H | E | R |
| | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
| | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 1 |
| | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 1 | 2 |
| | 4 | 5 | 6 | 7 | 1 | 2 | 3 |
| | 5 | 6 | 7 | 1 | 2 | 3 | 4 |
| | 6 | 7 | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| **Drop** | 7 | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 |

# Ratiba ya Kubadilishana Zamu kwa 2022-23

**2022-23**

**August**

| Mon | Tue | Weds | Thurs | Fri |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 8 | 9 | 10 | 11 | 12 |
| 15 | 16 | 17 | 18 | 19 |
| 22 | 23 | 24 | 25 | 26 |
| 29 P | 30 A | 31 N | 1 | 2 |

**September**

| Mon | Tue | Weds | Thurs | Fri |
|---|---|---|---|---|
| 29 | 30 | 31 | 1 T | 2 H |
| 5 | 6 E | 7 R | 8 P | 9 A |
| 12 N | 13 | 14 T | 15 H | 16 E |
| 19 R | 20 P | 21 A | 22 N | 23 T |
| 26 | 27 | 28 H | 29 E | 30 R |

**October**

| Mon | Tue | Weds | Thurs | Fri |
|---|---|---|---|---|
| 3 P | 4 A | 5 | 6 N | 7 T |
| 10 | 11 H | 12 E | 13 R | 14 P |
| 17 A | 18 N | 19 T | 20 H | 21 E |
| 24 R | 25 P | 26 A | 27 N | 28 T |
| 31 H | 1 | 2 | 3 | 4 |

**November**

| Mon | Tue | Weds | Thurs | Fri |
|---|---|---|---|---|
| | 1 E | 2 R | 3 P | 4 A |
| 7 N | 8 | 9 T | 10 H | 11 |
| 14 E | 15 R | 16 P | 17 A | 18 N |
| 21 T | 22 H | 23 | 24 | 25 |
| 28 E | 29 R | 30 P | | |

**December**

| Mon | Tue | Weds | Thurs | Fri |
|---|---|---|---|---|
| | | | 1 A | 2 N |
| 5 T | 6 H | 7 E | 8 R | 9 P |
| 12 A | 13 N | 14 T | 15 H | 16 E |
| 19 R | 20 P | 21 A | 22 N | 23 |
| 26 | 27 | 28 | 29 | 30 |

**January**

| Mon | Tue | Weds | Thurs | Fri |
|---|---|---|---|---|
| 2 | 3 T | 4 H | 5 E | 6 R |
| 9 P | 10 A | 11 N | 12 T | 13 H |
| 16 | 17 E | 18 R | 19 P | 20 A |
| 23 N | 24 T | 25 H | 26 E | 27 R |
| 30 P | 31 A | | | |

**February**

| Mon | Tue | Weds | Thurs | Fri |
|---|---|---|---|---|
| | | 1 N | 2 T | 3 H |
| 6 E | 7 R | 8 P | 9 A | 10 N |
| 13 T | 14 H | 15 E | 16 R | 17 P |
| 20 | 21 | 22 | 23 | 24 |
| 27 A | 28 N | | | |

**March**

| Mon | Tue | Weds | Thurs | Fri |
|---|---|---|---|---|
| | | 1 T | 2 H | 3 E |
| 6 R | 7 P | 8 A | 9 N | 10 T |
| 13 H | 14 E | 15 R | 16 P | 17 A |
| 20 N | 21 T | 22 H | 23 E | 24 R |
| 27 P | 28 A | 29 N | 30 T | 31 H |

**April**

| Mon | Tue | Weds | Thurs | Fri |
|---|---|---|---|---|
| 3 E | 4 R | 5 P | 6 A | 7 |
| 10 | 11 | 12 | 13 | 14 |
| 17 N | 18 T | 19 H | 20 E | 21 |
| 24 R | 25 P | 26 A | 27 N | 28 T |
| | | | | |

**May**

| Mon | Tue | Weds | Thurs | Fri |
|---|---|---|---|---|
| 1 H | 2 E | 3 R | 4 P | 5 A |
| 8 N | 9 T | 10 H | 11 E | 12 R |
| 15 P | 16 A | 17 N | 18 T | 19 H |
| 22 E | 23 R | 24 P | 25 A | 26 N |
| 29 | 30 T | 31 H | | |

**June**

| Mon | Tue | Weds | Thurs | Fri |
|---|---|---|---|---|
| | | | 1 E | 2 R |
| 5 P | 6 A | 7 N | 8 T | 9 H |
| 12 E | 13 R | 14 P | 15 A | 16 N |
| 19 | 20 T | 21 H | 22 | 23 |
| 26 | 27 | 28 | 29 | 30 |

# Huduma za Usaidizi wa Mwanafunzi

-Kabla na Baada ya Kufundisha shule - Zungumza na walimu wako kuhusu fursa hii

-Usuluhishi wa Rika - Kusuluhisha migogoro ndani ya kundi la wanafunzi; onana na Bw. Constant, Bw. Dion, au Bi. Sabater ili kujifunza zaidi

-Vikao vya Mduara vya Kurejesha Mahusiano - Kuimarisha mishikamano ya jamii na kurekebisha mahusiano; onana na Bw. Constant au Bw. Dion ili kujifunza zaidi

-Huduma za Usaidizi kwa Wanafunzi - Tafadhali tazama ukurasa wa chanjaa uliounganishwa ili kusoma zaidi kuhusu huduma mbalimbali zinazotolewa na Shule za Providence na jamii ili kuwasaidia wanafunzi kushinda vikwazo katika elimu yao

## Taarifa ya Mzazi

*Matarajio ya Wazazi Kulingana na Kanuni ya Maadili ya Shule ya Umma ya Providence:*

*Wanafunzi wana wajibu ku:*

- Kuhakikisha mtoto wao anafika shuleni kwa wakati, tayari kujifunza;
- Kuheshimu elimu ya mtoto wao na wataalamu wa shule;
- Kumsaidia mtoto wao kupanga kwa kila siku, wiki na mwaka shuleni;
- Kuomba msaada wakati hawawezi kukidhi mahitaji ya elimu ya mtoto wao; na
- Kuimarisha matarajio ya mwenendo wa Shule za Providence.

**Fursa kwa Ushirikishwaji;**
Baraza la Wazazi:
Shule ya E-Cubed siku zote inatafuta washirika wa wazazi ili watusaidie kuunda chama cha ushauri wa wazazi.chenye nguvu zaidi. Tafadhali dahili/uliza katika ofisi kuu au kwa simu namba 401-456-0694.

Wazazi na Timu ya Uboreshaji wa Shule (SIT)

Shule za Providence zinathamini na kuwakaribisha wazazi, familia, na wanajamii. Tunakukaribisha ujiunge na wafanyakazi wa shule ili kufanya kazi katika kuboresha ufaulu wa wanafunzi na pia kuongeza ushiriki wa wazazi kwa kushirikishwa katika Timu ya Uboreshaji ya Shule katika shule ya mwanafunzi wako. Kwa taarifa zaidi, tafadhali angalia Kiambatisho 8.

## Tuzungumze!

Tunakualika ututumie maswali yako, wasiwasi, mapendekezo, na au pongezi. Tafadhali bonyeza hapa ili kupata taarifa zaidi kuhusu "**Tuzungumze!**". Unapochagua E-Cubed kufanya ombi, utasikia majibu kutoka kwetu kwa wakati unaofaa.

Tunatarajia kwa hamu kusikia kutoka kwako!

## Serikali ya Wanafunzi na Baraza la Ushauri la Mkuu wa Shule

**Serikali ya Wanafunzi**

Wanachama wa baraza la wanafunzi watachaguliwa na wenzao, wakiwakilisha kila ngazi ya daraja kupitia mchakato wa uchaguzi wa haki na usawa. Wanachama wa Serikali ya Wanafunzi wana wajibu wa kutumikia Timu ya Uongozi ya Wanafunzi wa E-Cubed. Majukumu ni pamoja na kuwasiliana na wenzao kwa ushirikiano na timu ya Utamaduni wa Shule ili kuelewa mahitaji na matatizo ya wanafunzi. Viongozi waliochaguliwa ni kama wafuatao:

- **Maafisa Wanne wa Darasa la 12:** Wanafunzi hawa, waliochaguliwa na baraza zima la wanafunzi, watakutana mara moja kwa mwezi na Timu ya Utamaduni ya Shule na kuwasilisha mipango yao ya hafla mbalimbali za shule
- **Mabalozi Sita wa Madaraja (Wawili kwa kila Daraja) la 9, 10 na 11:** Wanafunzi hawa watachaguliwa na wanafunzi katika daraja zao, na watakutana mara moja kwa mwezi na Maafisa wa Daraja la 12 ili kujadili kile ambacho wangependa maafisa walete kwenye mkutano wao na Timu ya Utamaduni ya Shule

**Baraza la Ushauri la Mkuu wa Shule**

Baraza la Mkuu wa Shule ni timu inayoongozwa na wanafunzi ikiwa na mwanachama mmoja kutoka katika chombo cha Serikali ya Wanafunzi kwa kila ngazi ya darasa. Dhumuni la Baraza la Mkuu wa Shule ni kufanyia kazi yafuatayo:

- Kuendeleza msimamo mzuri kutoka kwa wanafunzi kwenda kwa jamii ya mtaa na ya shule.
- Kukuza morali ya shule na hali ya hewa
- Kutoa baraza kwa ajili ya sauti ya wanafunzi katika jamii ya shule
- Kuendeleza mahusiano mazuri miongoni mwa wanafunzi na kitivo
- Kusaidia kuratibu shughuli za wanafunzi

PANTHERS
E-CUBED ACADEMY
PROVIDENCE, RI

# Fomu ya Kukiri Kijitabu cha Mafanikio ya Mwanafunzi

Mimi, _____________________________________ (jina la mwanafunzi) nimesoma na nimeelewa matarajio na sera zote zilizoandikwa kikamilifu za Kijitabu cha Mwanafunzi.

Ninaelewa matarajio ya kiteknolojia, kitaaluma, kijamii, kitabia, kimichezo na mahudhurio na ninaahidi kuzingatia haya nikiwa kama Mwanafunzi wa E-Cubed.

Saini ya Mwanafunzi:________________________________________

Tarehe:__________